SHULE YA SEKONDARI SHEKILANGO

S.L.P 134

Barua pepe: shekilango2004@gmail.com

Mob 0714 874 399

Tarehe: 20 /12/2020

Kumb Na. SSS/S.1296/JI/021/VOL.I/001

Jina la Mwanafunzi: **.....**

S.L.P .....
MOMBO.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SHEKILANGO WILAYA YA KOROGWE MKOA WA TANGA MWAKA 2021

1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza (I) katika shule hii mwaka **2021** shule ya sekondari Shekilango ipo umbali wa meta 250 toka barabara kuu ya Tanga – Arusha katika mji mdogo wa Mombo, Wilaya ya Korogwe.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021** ndani ya siku saba.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 SARE ZA SHULE

Sare ya shule ni rangi ya damu ya mzee

A. WAVULANA

- Suruali mbili (2) zenye rinda mbili, zisizobana na mashati meupe mawili(2) aina ya “tetron-tomato”
- Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili (2) vya kupiga kiwi visivyo na visigino virefu wala urembo wowote vya kufunga kwa kamba.
- Soksi nyeusi jozi mbili (2)
- Sweta moja (1) rangi ya damu ya mzee
- Mkanda wa ngozi mweusi (usiwe na bakozi pana kuliko mkanda)
- Tisheti ya shule

Sare za michezo

(i) Track suti ya rangi nyeusi Adidasi juu na chini - **Wote.**
(ii) Bukta ya rangi nyeusi Adidasi - **Wote**
(iii) Raba - **Wote**
(iv) Viatu vya mpira wa miguu - **kwa wachezaji tu.**
(v) Soksi ndefu za michezo rangi nyeusi - **kwa wachezaji tu.**

B. WASICHANA

- Sketi mbili (2) za rinda boksi ziwe ndefu hadi kwenye kifundo cha mguu na mashati meupe mawili (2) aina ya "tetroni – tomato"
- Kwa wale watakaovaa Hijabu isiwe inabana mwili kuonyesha maumbile. Aina ya kitamba cha juba ni **"Halua"** (juba lifunike mikono ila mikono mifupi haitaruhusiwa)
- Soksi nyeupe ziwe ndefu, jozi mbili (2)
- Sweta moja (1) rangi ya damu ya mzee
- Viatu vyeusi jozi mbili (2) vya ngozi vya kupiga kiwi visivyo na visigino virefu wala urembo wowote vya kufunga na kamba.
- Tisheti ya shule

Sare za michezo

(i) Track suti ya rangi nyeusi Adidasi juu na chini **- Wote.**
(ii) Raba – **Wote.**
(iii) Viatu vya mpira wa miguu **- kwa wachezaji tu.**
(iv) Soksi ndefu za michezo rangi nyeusi **- kwa wachezaji tu.**

3.0 VIFAA VYA KUJIFUNZIA KWA WANAFUNZI WOTE

Mzazi/Mlezi hakikisha unampatia mwanao mahitaji yafuatayo:-

1. Daftari 12 (Counter books)
2. Begi 1 (mifuko ya rambo na mabegi yenye picha au maandishi yasiyo na maadili haviruhusiwi) Mfano:- picha ya jani la bangi.
3. Mkebe 1 (Mathematical set)
4. Kalamu, penseli na rula

4.0 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau Bendera ya Taifa

h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kuwa na simu ya mkononi

5.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi

i. Fomu namba – I. 'Medical Examination Form' ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
ii. Fomu namba – II.
(**a) Ahadi ya Mwanafunzi:-**
Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
(b) Ahadi ya Mzazi/ Mlezi:-
Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

6.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu na kwa wakati.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Ahsante.

……..

GEOFREY E. TEMBA
MKUU WA SHULE

Fomu Na. I

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

(Ijazwe na kurudishwa kwa mkuu wa shule)

SHEKILANGO SECONDARY SCHOOL

P.O.BOX 134

MOMBO

Date: 02/12/2019

To:

The medical officer

……
……
……
Mr./Ms./Miss ……..

Please examine the above named as to his fitness for enrollment as student on temporary/ permanent/ Contract terms.

Date: …… **Signature …….**

PART B

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by the medical officer)

I have examined the above named for secondary education

A. Eye sight _____
B. Hearing _____
C. Limbs _____
D. Venereal Diseases _____
E. Speech _____
F. Leprosy _____
G. Epilepsy _____
H. STD'S _____
I. Neuroses _____
J. Pregnancy _____
K. Other serious diseases _____

Station: ……. Designation: ……..……

Date: ……. Signature: …….

NAME: …… STAMP: ……....

SHULE YA SEKONDARI SHEKILANGO

(Ijazwe na kurudishwa kwa mkuu wa shule)

(a) AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi ……. Nimeyasoma na kuyaelewa maelekezo yote ambayo ni pamoja na sheria za shule na nimekubali kuingia kidato cha kwanza katika shule ya sekondari ya shekilango hadi nitakapo maliza kidato cha nne (iv)

Naahidi kwamba:

i. Nitasoma kwa bidii ili niweze kufaulu masomo yangu yote
ii. Nitahudhuria shule siku zote za masomo bila kukosa.
iii. Nitatii sheria zote za shule na kuzifuata kikamilifu. Nafahamu kwamba kitendo chochote kinyume na taratibu za shule kinastahili adhabu kali ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.
iv. Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na sheria za shule na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
v. Nitatunza mali za umma ambazo ni pamoja na majengo, samani, vitabu na vinginevyo.

……. **…….**

Tarehe **Sahihi ya mwanafunzi**

(b) AHADI YA MZAZI/ MLEZI

Mimi …… Mzazi/Mlezi wa ……..……

Naahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule na walimu wote kwa ujumla katika kumwelimisha na kumlea mtoto wangu hii ni pamoja na kuhakikisha kwamba

i. Mwanangu awapo shuleni awe anatii sheria zote za shule kikamilifu.
ii. Kufuatilia maendeleo ya mwanangu mfano: ripoti na masomo.
iii. Kuhudhuria vikao vyote vinavyoitishwa na uongozi wa shule.
iv. Kumwandalia mazingira mazuri ya kujifunzia, kumkagua, kumsimamia masomo awapo nyumbani.

Namba ya simu ya mzazi /mlezi: .....

Mahali anapoishi mzazi /mlezi: .....

…….. **……**

Tarehe **Sahihi ya mzazi/ mlezi**

…….. **……**

Tarehe **Sahihi ya mkuu wa shule.**